

WOSIA-JIBU*(Jibu la Yusufu Kalala Kuhusiana na Shairi la Wosia)*

1. Naitafuta johari, nipate kukupambia.
Nimelisoma shairi, ulilomuandikia.
Huyo nduguyo Bakari, apate kukusikia.
Wosia wa Bakari, sote unatufaa.
2. Umeandika vizuri, vina kuvipangilia.
Yale maonyo ya kheri, rahisi kuyatambua.
Kwa anaye fikiri, ni bora kuyafuatia.
Wosia wa Bakari, sote unatufaa.
3. Tuitumie khiari, na jitihada zetu pia.
Tusitafute fakhari, kuzidi kuangamia.
Si uamuzi mzuri, wa mtu kujivunia.
Wosia wa Bakari, sote unatufaa.
4. Naitafuta zumari, wimbo nitakuambia.
Umechoma msumari, kofia nakuvulia.
Hili ni jambo la kheri, mwenzio kumtakia.
Wosia wa Bakari, sote unatufaa.

*Yusuf Kalala. (Washington, DC).
Julai, 2002*